**HEALTHY BIRTH DAY, INC.**

**(*inayoitwa pia* COUNT THE KICKS)**

**MASHARTI YA MATUMIZI**

Kuanza kutumika tarehe 9 Julai, 2018.

**Utangulizi**

Maazimio ya shirika lisilo la kiserikali la 501(c)(3) liitwalo Healthy Birth Day, Inc. ni kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya watoto wanaozaliwa wakiwa tayari wamefariki kwa kutumia kampeni ya kuhamasisha kuhusu afya ya umma ya Kuhesabu Kusoga kwa mtoto. Count the Kicks huelimisha wanawake wanaoelekea kujifungua kuhusu umuhimu wa, na mbinu ya, kufuatilia kusoga kwa kijusi katika wiki kumi za mwisho za ujauzito. Wanawake wajawazito wana uwezo wa kuwaokoa watoto wao kwa kufahamu utaratibu wa kusoga kwa watoto wao na kujihisi wamewezeshwa kuwajulisha daktari wao wanapogundua badiliko. Masharti yafuatayo ya Matumizi yatadhibiti utumiaji wako wa programu ya Count the Kicks.

**Kukubali Masharti ya Matumizi**

Masharti haya ya matumizi ni makubaliano ya, na kati ya Wewe na Kampuni, washirika na tanzu zake ("**Kampuni**" au "**sisi**"). Sheria na masharti yafuatayo, pamoja na hati zozote ambazo yanajumuisha kwa uwazi kwa kuzirejelea (pamoja, "**Masharti** haya ya **Matumizi**"), yanadhibiti ufikiaji na matumizi yako ya programu yetu ya Count the Kicks ("**Programu yetu**" ikiwemo maudhui, matumizi na huduma zozote zinazotolewa kwenye au kupitia kwa Programu au Tovuti ya Count the Kicks, www.countthekicks.org.

Tafadhali soma Masharti ya Matumizi kabla ya kuanza kutumia Programu. Kwa kutumia Programu au kwa kubofya ili kukubali au kuitikia Masharti ya Matumizi wakati chaguo hili limetolewa, unakubali na kuitikia kuwa utadhibitiwa na utazingatia Masharti haya ya Matumizi na Sera yetu ya Ufaragha, inayopatikana hapa, iliyojumuisha hapa kwa kurejelewa. Ikiwa hutaki kukubali Masharti haya ya Matumizi au Sera ya Ufaragha, ni lazima usifikie wala kutumia Programu.

Programu hii inatolewa na inapatikana kwa watumiaji wenye umri wa miaka 16 au zaidi. Kwa kutumia Programu hii, unawakilisha na kuthibitisha kuwa unatimiza matakwa yote ya kustahiki kabla ya matumizi. Ikiwa hutimizi matakwa haya yote, ni lazima usifikie wala kutumia Programu.

Kwa ajili ya Kanuni ya Ulinzi wa Data ya Jumla, Mdhibiti wa Data na Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya (EU) ni QCI ya West Des Moines, Iowa, ambayo taarifa zake za mawasiliano zinaweza kupatikana hapa chini.

Katika Masharti haya yote ya Matumizi, tunatumia neno "**Nchi Teule**" kurejelea nchi zilizoko kwenye Umoja wa Ulaya (EU), Eneo la Kibiashara la Ulaya, (EEA), na Uswizi. Ikiwa unaishi katika Nchi Teule, una haki kadhaa ambazo tunataka uzifahamu. Haki hizi zitaonyeshwa kwa kurejelea Nchi Teule pale zinatumika.

**Mabadiliko ya Masharti ya Matumizi**

Tunaweza kubadilisha na kusasisha Masharti haya ya Matumizi mara kwa mara kufuatia uamuzi wetu pekee. Mabadiliko yote huanza kutumika mara moja tunapoyachapisha na yanatumika kwa ufikiaji na matumizi yote ya Tovuti hapo baadaye. Tukifanya mabadiliko makubwa ya Masharti haya ya Matumizi,

tutakupa notisi kupitia kwa Tovuti na Programu yetu, au kupitia mbinu zingine, ili kukupa fursa ya kupitia mabadiliko kabla ya kuanza kutumika.

Kuendelea kutumia Programu baada ya kuchapishwa kwa Masharti ya Matumizi yaliyorekebishwa kunamaanisha unakubali na unaitikia mabadiliko. Unatarajiwa kupitia ukurasa huu mara kwa mara ili ufahamu mabadiliko yoyote, kwa sababu yanatumika kwako.

**Wajibu**

Hizi hapa ni baadhi ya ahadi ambazo unatoa kwetu unapokubali Masharti haya ya Matumizi:

**Akaunti Yako**

Ukiamua kufungua Akaunti kwenye Programu yetu, unakubali yafuatayo:

- Nywila yako itakuwa siri.
- Hutashiriki Akaunti na mtu mwingine yeyote na utafuata kanuni zetu, ikiwemo lakini sio tu Masharti haya ya Matumizi na Sera yetu ya Ufaragha, na sheria.
- Unawajibikia kitu chochote kinachotokea kupitia kwa Akaunti yako isipokuwa ukiifunga au uripoti matumizi mabaya.
- Unakubali kuwa taarifa iliyotolewa kwenye programu ni kwa ajili ya matumizi ya kielimu pekee na hainuiwi kutumiwa katika ugunduzi au matibabu. Taarifa hii inapaswa kutumiwa kwa mujibu wa mtoa huduma wako wa afya.

**Notisi na Ujumbe**

Kwa kufikia Programu yetu, unakubali yafuatayo:

- Unakubali tukutumie ntoisi an ujumbe kuhusu programu au huduma zetu. Ikiwa taarifa yako ya mawasiliano haijasasishwa, unaweza kukosa kupokea notisi muhimu.
- Unakubali kuwa tutakutumia notisi na ujumbe kwa njia zifuatazo: (1) kwenye Programu, au (2) tukutumie kwa taarifa ya mawasiliano uliyotupa (k.m., barua pepe, nambari ya simu ya mkono, anwani ya mahali unapoishi). Unakubali kusasisha taarifa yako ya mawasiliano.
- Unakubali kuwa Healthy Birth Day, Unc., ikiwa na maazimio ya kuzuia kuzaliwa kwa watoto ambao tayari wamefariki na kuokoa watoto, inaweza kutumia data yako uliyohesabu mtoto akisoga katika uchunguzi, tathmini au tafiti ikiwa na lengo la kuboresha programu yetu na kuimarisha ufanisi wake.

**Haki na Mipaka**

**Unamiliki taarifa yako**

Unamiliki maudhui, maoni, na taarifa yote binafsi unayotoa kwetu. Tutaheshimu uamuzi unaofanya kuhusu jinsi tunatumia taarifa yako. Wewe na Kampuni mnakubali kuwa ikiwa taarifa yoyote yako inajumuisha data ya mtu binafsi, inadhibitiwa na Sera yetu ya Ufaragha.

Wewe na Kampuni mnakubali kuwa tunaweza kufikia, kuhifadhi, kuchakata na kutumia taarifa yoyote na data ya mtu binafsi unayotoa kulingana na masharti ya Sera yetu ya Ufaragha.

Unakubali kutoa tu taarifa ambayo haikiuki sheria wala haki za mtu yeyote (zikiwemo hakimiliki za ubunifu). Unakubali pia kuwa taarifa unayotoa itakuwa ya kweli. Kampuni inaweza kuhitajika kisheria kuondoa taarifa fulani.

**Maudhui, Tovuti na Programu Zingine**

Unapotumia Programu au huduma zetu, unaweza kukumbana na maudhui au taarifa ambazo zinaweza kuwa si sahihi, hazijakamilika, zimechelewa, zinapotosha, si halali, zinaudhi au vinginevyo za kuumiza. Hatuwezi kuzuia matumizi haya mabaya ya huduma zetu kila wakati, na unakubali kuwa hatuwajibikii matumizi mabaya kama hayo.

Una wajibu wa kuamua ikiwa unataka kufikia au kutumia programu au tovuti tusizomiliki ambazo zinaweza kuunganishwa kutoka kwa Tovuti au huduma zetu,. Ukikubali programu au tovuti tusiyomiliki kukuthibitisha, programu au tovuti hiyo inaweza kufikia taarifa inayohusiana na wewe. Programu na tovuti tusizomiliki zina masharti yao ya kisheria na sera za faragha, na unaweza kuwa unawapa wengine idhini ya kutumia taarifa yako kwa njia ambazo hatungetumia. Isipokuwa kwa kiwango kidogo ambacho inaweza kuhitajika na sheria husika, Kampuni haiwajibikii tovuti na programu hizi—zitumie kwa tahadhari. Tafadhali angalia Sera yetu ya Ufaragha.

**Mipaka**

Kampuni ina haki ya kukuwekea mipaka matumizi ya Programu au huduma zetu, ikiwemo idadi za miunganisho. Kampuni ina haki ya kuzuia, kusitisha, au kukomesha Akaunti yako ikiwa Kampuni inaamini umekiuka Masharti haya ya Matumizi, Sera yetu ya Faragha, au sheria au unatumia vibaya Tovuti au huduma zetu.

**Hakimiliki za Ubunifu**

Kampuni ina miliki haki zake zote za ubunifu katika Porgramu na huduma zetu. Kutumia Programu au huduma hakukupi umiliki wowote wa huduma au maudhui au taarifa zetu zinazotolewa kupitia kwa Programu au huduma zetu. Alama za biashara na nembo zinazotumiwa kuhusiana na Programu au huduma ni alama za biashara za wamiliki wake.

**Uchakataji wa Kiotomatiki**

Tutatumia taarifa na data unayotoa na tunayopokea kukuhusu ili kutoa mapendekezo ya miunganisho, maudhui na vipengee ambavyo vinaweza kukusaidia. Kwa mfano, tunaweza kutumia data na taarifa kukuhusu ili kukupendekezea bidhaa. Kuweka taarifa yako ikiwa sahihi na imesasishwa hutusaidia kukupa mapendekezo ambayo ni sahihi na yanakufaa zaidi.

**Kanusho na Upeo wa Dhima**

**Hakuna Udhamini**

KWA KIWANGO KINACHOKUBALIWA NA SHERIA, KAMPUNI NA WASHIRIKA WAKE (NA WALE AMBAO KAMPUNI HUFANYA KAZI NAO ILI KUTOA HUDUMA) (A) WANAKANUSHA UDHAMINI NA UWAKILISHI WOTE UNAODOKEZWA (K.M. UDHAMINI WA MAUZO, UFAAFU KWA LENGO FULANI, USAHIHI WA DATA, NA KUTOINGILIWA); (B) HAWATHIBITISHI KUWA HUDUMA ZITATOLEWA BILA

KUVURUGWA AU MAKOSA, NA (C) KUTOA HUDUMA (IKIWEMO MAUDHUI NA TAARIFA) KULINGANA NA “JINSI ILIVYO” NA WAKATI ‘INAPOPATIKANA”.

SHERIA ZINGINE HAZIRUHUSU KANUSHO FULANI, KWA HIVYO BAADHI YA AU KANUSHO HIZI ZOTE ZINAWEZA KUKOSA KUTUMIKA KWAKO.

**Kutotumika kwa Dhima**

KWA KIWANGO KINACHOKUBALIWA NA SHERIA (NA ISIPOKUWA PALE AMBAPO KAMPUNI INA MKATABA TOFAUTI AMBAO UNAZIDI KANDARASI HII), KAMPUNI NA WASHIRIKA WAKE (NA WALE AMBAO KAMPUNI HUFANYA KAZI NAO ILI KUTOA HUDUMA) HAITAKUWAJIBIKIA AU KUWAJIBIKIA WENGINE KWA UHARIBIFU USIO WA MOJA KWA MOJA, USIOTARAJIWA, MAALUM, UNAOSABABISHWA NA MATOKEO AU ADHABU, KUPOTEA KOKOTE KWA DATA, FURSA, SIFA, FAIDA AU MAPATO, YANAYOHUSIANA NA HUDUMA (K.M. KAULI ZA MATUSI AU KUCHAFULIWA JINA, KUVURUGWA KWA KAZI AU KUPOTEA, MATUMIZI YA, AU MABADILIKO YA, TAARIFA AU MAUDHUI YAKO).

KATIKA HALI YOYOTE DHIMA YA KAMPUNI NA WASHIRIKA WAKE (NA WALE AMBAO KAMPUNI HUFANYA KAZI NAO ILI KUTOA HUDUMA) HAITAZIDI, KWA JUMLA YA MALIPO YOTE, KIASI AMBACHO KIKO CHINI YA (A) MARA TANO YA ADA YA HIVI KARIBUNI ZAIDI YA KILA MWEZI AU KILA MWAKA AMBAYO ULILIPIA HUDUMA, IKIWA KUNAYO YOYOTE, AU (B) DOLA ZA MAREKANI $1000.

UPEO HUU WA DHIMA NI SEHEMU YA MSINGI WA MAKUBALIANO BAINA YAKO NA KAMPUNI NA UTATUMIKA KWA MALIPO YOTE YA DHIMA (K.M. UDHAMINI, KOSA LA DAAWA, UPUUZAJI, KANDARASI, SHERIA) NA HATA KAMA KAMPUNI AU WASHIRIKA WAKE IMEARIFIWA KUHUSU UWEZEKANO WA UHARIBIFU WOWOTE KAMA HUO, NA HATA KAMA SULUHU HIZI HAZITIMIZI LENGO LAKE.

SHERIA ZINGINE HAZIRUHUSU KUWEPO NA UPEO AU KUTOJUMUISHWA KWA DHIMA, KWA HIVYO MIPAKA HII INAWEZA KUKOSA KUTUMIKA KWAKO.

**Usitishaji**

Wewe na Kampuni mnaweza kusitisha makubaliano yenu chini ya Masharti haya ya Matumizi wakati wowote kwa kupeana notisi kwa nyinyi wenyewe. Baada ya kusitishwa, unapoteza haki ya kufikia au kutumia huduma. Yafuatayo yataendelea hata baada ya kusitisha makubaliano:

- Haki zetu za kutumia na kufichua maoni yako;
- Vifungu vifuatavyo vya Masharti yetu ya Matumizi: Kanusho na Upeo wa Dhima; Sheria Inayodhibiti na Usuluhishaji wa Ugomvi; na Masharti ya Jumla;
- Kiasi chochote cha fedha zinazodaiwa na mmojawapo wa wahusika kabla ya kusitishwa kwa makubaliano kinasalia kudaiwa hata baada ya makubaliano kusitishwa.

Ikiwa ulifungua Akaunti, unaweza kuwasiliana nasi kwa kutumia Taarifa zetu za Mawasiliano zilizo hapa chini ili kufunga Akaunti yako.

**Sheria Inayodhibiti na Usuluhishaji wa Ugomvi**

Ikiwa itatokea tukio la kusikitisha ambapo tutakuwa na ugomvi wa kisheria, wewe na Kampuni mnakubali kusuluhisha katika korti za Iowa kwa kutumia sheria ya Iowa, au korti za Marekani kwa kutumia sheria ya Marekani.

**Masharti ya Jumla**

Ikiwa korti yenye mamlaka yanayozidi Masharti haya ya Matumizi itapata sehemu yoyote yake ikiwa haiwezi kutekelezwa, wewe na sisi tunakubaliana kuwa korti inapaswa kurekebisha masharti ili kufanya sehemu hiyo iweze kutekelezwa huku bado ikitimiza lengo lake. Ikiwa korti haiwezi kufanya hivyo, wewe na sisi tunakubali kuisihi korti kuondoa sehemu hiyo isiyoweza kutekelezwa na bado itekeleze Masharti ya Matumizi yaliyosalia.

Ikiwa hatutachukua hatua kufuatia ukiukaji wa Masharti haya ya Matumizi, hiyo haina maana kuwa tumeondoa haki yetu ya kutekeleza Masharti haya ya Matumizi. Usipeane au kuhamisha haki zako chini ya Masharti haya ya Matumizi kwa mtu yeyote bila kibali chetu. Hata hivyo, unakubali kuwa tunaweza kupeana haki zetu chini ya Masharti haya ya Matumizi kwa washirika wetu au mhusika ambaye atanunua Kampuni bila idhini yako. Hakuna wahusika wa tatu wanaofaidika na Masharti haya ya Matumizi.

Unakubali kuwa njia pekee ya kutupa notisi ya kisheria ni kupitia kwa anwani zilizopeanwa katika sehemu ya “Taarifa ya Mawasiliano” iliyo hapa chini.

**Taarifa ya Mawasiliano**

Maswali, maoni na maombi yote kuhusiana na Masharti haya ya Matumizi yanapaswa kutumwa kwa:

Healthy Birth Day, Inc.
Ionekane na: Mkurugenzi Mtendaji
S.L.P. 71093, Clive, IA 50325 USA
1.515.523.5666
info@countthekicks.org

Kwa ajili ya Kanuni ya Ulinzi wa Data ya Jumla, wakaazi wa Nchi Teule wanaweza kuwasiliana na Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya (EU) wakiwa na maswali, maoni na maombi yote kuhusu Masharti haya ya Matumizi:

QCI
Ionekane na: Muundaji wa Programu ya Count the Kicks
4300 Westown Pkwy Ste 150, West Des Moines, IA 50266
1.515.440.4960
sfinn@qci.com